


D.C.T MVUMI SECONDARY SCHOOL



P.O. Box 62,
MVUMI,
DODOMA.

Phone: 0732 – 961171
Headmaster: 0717 – 245451
www.dctmvumi.sc.tz
E-Mail: dctmvumiss@gmail.com

TAARIFA MUHIMU KWA WAZAZI (A - LEVEL)

Kwa Niaba ya shule Napenda kuwasalimu Wote katika Jina la Bwana wetu Yesu Kristo. Zifuatazo ni taarifa muhimu kwa Mzazi/Mlezi.

I: RATIBA YA MIHULA (KUFUNGA NA KUFUNGUA) 2017/2018

MIHULA	KUFUNGUA	LIKIZO FUPI		KUFUNGA	IDADI YA SIKU
		KUFUNGA	KUFUNGUA		
MHULA 1	3/7/2017	1/9/2017	18/9/2017	8/12/2017	103
MHULA 2	8/1/2018	24/3/2018	09/4/2018	1/6/2018	91
JUMLA YA SIKU ZA MASOMO					194

NB: Mhula mpya wa Masomo utanza 2/7/2018.

II: KARO

Karo ilipwe kupitia benki kwenye akaunti zifuatazo:

CRDB Bank akaunti namba 0150447830600, Jina la akaunti ni D.C.T Mvumi Secondary School, Au NMB Bank, akaunti namba 52010017604, Jina la akaunti ni DCT Mvumi Secondary School. Jina la mwanafunzi na kidato liandikwe kwenye pay in slip (fomu ya kuweka fedha) na mwanafunzi aje nayo shuleni). (Kwa ufafanuzi zaidi wasiliana na Mhasibu wa Shule (0754 919 839 – 0715 919 839 au 0783 727 424)

III. MCHANGANUO WA MALIPO YA ADA (KARO) MWAKA 2017/2018

S/No.	Tarehe	Kutwa	Bweni
1	July 2017	575,000/=	1,115,000/=
2	January, 2018	510,000/=	1,050,000/=
	Jumla	1,085,000/=	2,165,000/=

IV. MAENDELEO YA MWANAFUNZI

Ni muhimu kila mzazi kufuatilia maendeleo ya kijana wake Kitaaluma, Kinidhamu na kuhakikisha unapata ripoti ya matokeo kila muhula, pia kuhudhuria vikao vya Wazazi au kuwasiliana na Mkuu wa Shule moja kwa moja au Mwalimu wa darasa ili kuulizia taarifa hizo.

V. SUMMER SCHOOL (Masomo wakati wa likizo)

Kutakuwa na masomo ya wakati wa likizo kwa madarasa ya mitihani, yaani kidato cha pili, cha nne na cha sita wakati wa likizo ndefu mwezi wa sita, ni muhimu kwa kila mtoto

kuhudhuria. Kama mtoto wako ni wa kidato cha II, IV au VI anatakiwa kuja na ada nyingine ya masomo ya likizo, ambayo hufanyika kila mwaka wakati wa likizo ya mwezi wa sita, wao hubaki na kufundishwa masomo yote.

Mchanganuo wa gharama za masomo wakati wa likizo ni kama ifuatavyo:-

- (i) Mwanafunzi wa bweni **Tshs. 125,000/=**
- (ii) Mwanafunzi wa kutwa **Tshs. 65,000/=**

Masomo ya likizo (Summer School) ni lazima kwa wanafunzi wetu wa DCT kwani ina malengo yafuatayo:-

- (a) Kuongeza ufanisi jinsi ya kujibu maswali, hasa yale wanayouliza walimu na Baraza la mitihani. (NECTA)
- (b) Kuwapa ujuzi na maarifa kwenye masomo yote.
- (c) Kumalizia mada zilizobaki kwenye silabasi.
- (d) Kuongeza kiwango cha kufaulu mitihani ya taifa.
- (e) Kuongeza uwezo binafsi wa kuelewa wa mwanafunzi kwa kutatua maeneo magumu wanayopata tabu wanafunzi wakati wa kujibu mitihani.

Wanafunzi wa shule zingine kidato cha Pili, cha Nne na cha Sita wote wanakaribishwa.

VI. PRE FORM FIVE

Kutakuwa na masomo kabla ya kuanza kidato cha Tano ambayo yataanza tarehe 1/4/2018 mpaka tarehe 31/5/2018 muda wa miezi miwili (2).

Mchanganuo wa gharama za masomo hayo ni kama ifuatavyo:-

- (i) Mwanafunzi wa bweni **Tshs. 250,000/=**
- (ii) Mwanafunzi wa kutwa **Tshs. 100,000/=**

VII. PRE FORM ONE

Kutakuwa na masomo kabla ya kuanza kidato cha kwanza ambayo yataanza katikati ya mwezi wa kumi (10) mpaka mwezi wa kumi na mbili (12) muda wa takriban miezi miwili na nusu.

Mchanganuo wa gharama za masomo hayo ni kama ifuatavyo:-

- (i) Mwanafunzi wa bweni **Tshs. 200,000/=**
- (ii) Mwanafunzi wa kutwa **Tshs. 80,000/=**

VIII. MAAGIZO MENGINE

1. Mwanafunzi anatakiwa awe na sare kamili ya shule (uniform, shamba dress na nguo za michezo) na hatakiwi kuja shuleni na nguo nyingine zozote zisizo sare ya shule.
2. Matibabu yatagharamiwa na mzazi nje ya ada. Unashauriwa kuleta **shs 30,000** au zaidi kila muhula kwa ajili ya matibabu ambazo zitahifadhiwa na shule na kutumiwa na mwanafunzi kwa ajili ya matibabu pindi auguapo na endapo hazitatumika zitarudishwa kwa mwanafunzi amalizapo shule. AU Mzazi/Mlezi Unashauriwa kumkatia bima ya afya mwanao.
3. Shule haina Utaratibu wa kutoa chakula special kwa wanafunzi wenye matatizo mabalimbali ya kiafya. Gharama hizo zitagharamiwa na mzazi au mlezi wa mwanafunzi husika.

Asante,

Malugu, F. A.
MKUU WA SHULE